SOMO LA PILI



YESU ALIFUNDISHA NINI?

Tafadhali andika jina lako hapo juu kisha jaza nukuu za Biblia katika nafasi zilizotolewa.

ALIFUNDISHA JUU YA UPENDO WA MUNGU KWA WENYE DHAMBI

Mwalimu mwema

Unakumbuka walimu uliokuwa nao shuleni? Wengine wao walikuwa wema- nawe ukajifunza mengi kutoka kwao. Yesu alikuwa mwalimu mwema.[1] Mara kwa mara alitumia mifano katika mafundisho Yake. Mifano ni habari nzuri zinazosisimua zenye maana zilizojificha.

Mifano mitatu ya Yesu ililinganishwa na watu wenye dhambi, kama sisi, kwa vitu ambavyo vilipotea na kufurahia kwa kuvipata.[2] Mafundisho ya mifano yote mitatu iko wazi. Kuna furahia mbinguni wenye dhambi *waliopotea* wanaporudi "nyumbani" kwa Mungu.

MUNGU HUWATAFUTA WENYE DHAMBI WALIOPOTEA

Mfano wa kwanza ni juu ya kondoo aliyepotea ambaye mchungaji alienda kumtafuta na kumpata. Mfano huu (na mwingine baada yake) inaongea juu ya Mungu kuwatafuta wenye dhambi, siyo wenye dhambi wakimtafuta.[3] Soma Luka 15:3-7. Andika mstari wa 6

.....

.....

.....

.....

Kondoo aliyepotea amepatikana

Yesu ni kama huyu mchungaji. Angalia Luka 19:10

.....

.....

MUNGU ANAWAKARIBISHA WENYE DHAMBI WALIOPOTEA

Mfano wa tatu ni juu ya mwana aliyeishi maisha mabaya sana ya anasa. Alipoikabidhi dhambi yake, babaye alimkaribisha nyumbani. Kijana huyu alikuwa amepoteza matumaini ya maisha yake. Mungu anafananishwa na huyu baba katika mfano huu. Tunapozikiri dhambi zetu, Mungu kwa furaha hutukaribisha tena tumrudie. Soma Luka 15:21-24. Andika mstari wa 24

Mwana mpotevu anarudi nyumbani

.....

.....

.....

Mfano huu unatufundisha juu ya toba. Toba ni kuiacha dhambi na kumrudia Mungu. Tutaliangalia hili zaidi tutakapoingia somo la 6.

---

[1] Yesu alifundisha kwa mamlaka (Luka 4:32) na alitamaniwa na wasikilizaji Wake (Luka 4:22).

[2] Luka 15:1-7 (Kondoo aliyepotea), 8-10 (Shilingi iliyopotea), 11-32 (Mwana mpotevu).

[3] Wenye dhambi watabaki wamepotea, labda Mungu achague kuwatafuta na kuokoa baadhi. Angalia Waefeso 1:4.

Sasa tazama aina nyingine ya mafundisho Yake.

Sheria za furaha

ALIELEZEA SHERIA YA MUNGU

Sheria za kibinadamu zimekusudiwa kutengeneza aina ya maisha kuwa ya furaha. Sheria inayotuambia kuwa tubakie sehemu moja ya barabara huzuia ajali. Na sheria zinazozuia wizi huhifadhi mali zetu. Sheria za Mungu pia zimekusudia furaha kwa ajili yetu. Lakini kipimo cha Mungu ni cha juu kuliko vipimo vyetu.

YESU ALIFUNDISHA KUWA NI LAZIMA TUWE WAKAMILIFU

Alifundisha kuwa ni lazima tuwa wema kama Mungu alivyo. Hili linaweza kusikika visivyo (na ni kweli), lakini ndivyo tulivyotakiwa kuwa tangu mwanzo. Angalia Mathayo 5:48

.....

.....

YESU ALIFUNDISHA KIWANGO CHA SHERIA YA MUNGU

Alituonyesha kuwa sheria ya Mungu hufunika kila kitu tunachofikiri na kusema, pia na hata tufanyacho.[4] Angalia Mathayo 5:28

.....

.....

.....

YESU ALIFUNDISHA UMUHIMU WA UPENDO

Yesu alisema kama *tunampenda* Mungu na watu kama tunavyojipenda basi tutafanya yale sheria ya Mungu inayohitaji.[5] Tunaweza *kufikiri* kuwa tunampenda kila mmoja, lakini je tunawapenda adui zetu?
Angalia Mathayo 5:44

Upendo kwa adui

.....

.....

.....

.....

Atateseka msalabani!

ALIFUNDISHA KUWA NI LAZIMA TUTESEKE

Wote tunajua kuwa ni lazima tutakufa siku moja. Lakini hatuzaliwi na kusudi la kufa. Tunazaliwa ili tuweze kuishi maisha marefu. Kifo ni bahati mbaya isiyokaribishwa!

Yesu, kwa sehemu nyingine, aliongelea kama kifo Chake ndicho kilichokuwa sababu ya msingi ya kuzaliwa Kwake. Aliona kifo cha ukaidi cha kusulubiwa; moja ya kifo cha maumivu na aibu ambacho mtu asingependa kukifikia. Ulikuwa unabii wa ajabu sana. Kwa nini kila mmoja ategemee kumuua mtu mwema kama Yesu? Pia alitabiri kuwa atakuwa hai ndani ya siku tatu baada ya kufa Kwake.

[4] Mathayo 5:21-22 na 27-28.
[5] Mathayo 22:36-40.

YESU ALISEMA ALIZALIWA KWA KUSUDI LA KUFA

Alisema ilikuwa muhimu Kwake kufa na kuwa hai tena. Aliwaambia wanafunzi wake juu ya hili kwa matukio matatu.[6]
Angalia Mathayo 16:21

Alizaliwa ili kufa

.....

.....

.....

.....

.....

YESU ALISEMA ATAKUFA KWA AJILI YA KONDOO WAKE

Katika siku za Yesu, mchungaji mwema angetoa maisha yake kwa ajili ya kuokoa kondoo wake kutoka kwa mbwa-mwitu. Yesu akasema Atakufa kwa ajili ya *kondoo Wake* (yaani waumini). Alitabiri siku ambayo atatoa maisha Yake kwa niaba ya kondoo Wake. Angalia Yohana 10:11

Mchungaji wa mashariki

.....

.....

Mwisho, Yesu alisema kifo Chake kilikuwa ni "fidia kwa wengi".[7] Na masaa machache kabla ya kufa Kwake, aliwafundisha wanafunzi wake somo la mfano kwa kutumia mkate na divai. Aliongea nao kama viwakilishi vya mwili na damu Yake. Vilitakiwa kuchukuliwa kama kumbukumbu ya kifo cha upendo Wake kwao.[8]

Tutaangalia katika somo la 4 maelezo yaliyotolewa na waandishi wa Agano Jipya juu ya kifo cha Yesu.

ALISEMA ATARUDI KUHUKUMU



Kuwahukumu watenda maovu

Popote palipo na sheria pana adhabu kwa wasiozitii sheria. Lakini wale waliochaguliwa kuhukumu siyo wakamilifu wenyewe. Na kwa sababu siyo wakamilifu, watafanya makosa – wasio na hatia wakati mwingine wataonewa, na wenye hatia wataachiwa huru.

Mahakimu wa duniani huhusika zaidi na dhambi za wazi kama za wizi, ugomvi, uonevu, nk. Lakini dhambi zilizojificha kama chuki, uchafu, na ubinafsi/unafiki, hazihukumiwi na watu. Kama mtu angechaguliwa kuhukumu wengine kwa dhambi *hizi* angehitajika asiwe mtu mwenye hatia mwenyewe.

Makosa yote ni dhambi machoni pa Mungu, na yanastahili kuhukumiwa. Lakini ni nani mkamilifu kabisa asiye na dhambi afanye jukumu hili? Ni nani aliye mkamilifu kabisa atakayehukumu kwa haki? Ni nani anayeelewa mwenye elimu yote awezaye kuhusika na matukio yote ambayo hutufanya tutende jinsi tutendavyo? Yesu ndiye mtu pekee mwenye sifa timilifu; hakuna mtu wa kawaida aliye mwema kama Yeye, angalia aliyoyasema Yesu katika somo hili.

Mhukumu wa haki

[6] Mathayo 16:21, 17:22-23 na 20:18-19.
[7] Marko 10:45 (angalia somo la 4).
[8] Luka 22:19-20.

Heshima kuu/kubwa

YESU ALISEMA AMECHAGULIWA KUWA MHUKUMU WA ULIMWENGU

Heshima hii kuu, Yesu alisema, ilitolewa Kwake na Mungu – Baba Yake wa Mbinguni. Angalia Yohana 5:22-23

.....

.....

.....

.....

.....

Mungu-Mwanadamu anaweza kuona vitu vyote kutoka sehemu zote.

Yesu alisema Yeye ni "Mwana wa Adam" lakini pia ni "Mwana wa Mungu". Kwa kusema hivi, alijishuhudia Mwenyewe kuwa mwanadamu halisi. Kama mwanadamu alipatwa na majaribu na magumu yanayowapata wanadamu wote. Kama mwanadamu asiye na dhambi,[9] Alielewa kwa uhakika, na atahukumu kwa haki. Angalia Yohana 5:26-27

.....

.....

.....

.....

YESU ALISEMA ATAUHUKUMU ULIMWENGU ATAKAPORUDI

Yesu hakusema kuwa Atauhukumu ulimwengu kwa haraka. Alisema Hakuja kuuhukumu, bali kuuokoa.[10] Lakini aliosema juu ya siku Atakayorudi kuuhukumu. Mataifa yote yatakusanyika mbele zake Naye atawabagua waliookoka kutoka kwao wasiookoka. Angalia Mathayo 25:31-32

Yesu anarudi tena

.....

.....

.....

.....

.....

.....

NA MWISHO

Yesu hakumaanisha ataendelea kuzaliwa tena na tena

Yesu akasema juu ya hitaji la mabadiliko ya ndani ambayo yangepatikana kwa Roho wa Mungu tu. Mabadiliko haya yalikuwa ya ndani sana ambayo Aliyalinganisha na kuzaliwa mara ya pili. Bila mabadiliko haya ilikuwa haiwezekani, kuingia mbinguni, Alisema.[11] Je umewahi kuyapata mabadiliko haya? Kama umeyapata mabadiliko haya utataka kuyafuata mafundisho ya Yesu yaliyoelezewa katika somo hili.

[9] Angalia somo la 3.
[10] Yohana 12:47.
[11] Yohana 3:3-5.